**MAMLAKA YA MAENDELEO YA BIASHARA TANZANIA (TANTRADE)**

**MWONGOZO WA USHIRIKI WA TANZANIA KATIKA MAONESHO YA KIMATAIFA YA MAZAO YA KILIMO (HORTICULTURAL EXPO DOHA 2023) YATAKAYOFANYIKA TAREHE 2 OKTOBA, 2023 HADI 28 MACHI, 2024 NCHINI QATAR.**

## 1.0 UTANGULIZI

Wizara ya Viwanda na Biashara kupitia Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade) inaratibu ushiriki wa Tanzania katika Maonesho ya Kimataifa ya Mazao ya kilimo (Holticuluture Expo Doha 2023) yanayotarajiwa kufanyika kuanzia tarehe 2 Oktoba, 2023 hadi 28 Machi, 2024 Doha, Qatar. Maonesho hayo yameandaliwa kwa ajili ya kuwakutanisha na kuwapa fursa wakulima na wazalishaji wa bidhaa za matunda, viungo na mbogamboga kote duniani kuonesha, kutangaza na kukuza bidhaa zao katika masoko ya kimataifa pamoja na kujifunza masuala mbalimbali ikiwemo teknolojia ya uzalishaji na usindikaji bora wa mazao hayo katika kuongeza thamani.

Expo Doha 2023 ni Maonesho ya kwanza kufanyika katika nchi yenye Mazingira ya jangwa. Maonesho haya ni kuzikutanisha nchi washiriki kutoka sehemu mbalimbali duniani ili kujadili na kutafuta ufumbuzi wa changamoto za kilimo kwenye mazingira ya Jagwa.

## KAULI MBIU YA EXPO DOHA 2023

Kauli mbiu ya Expo Doha 2023 ni **Jangwa la Kijani, Mazingira Bora (Green Desert, Better Environment)** ambayo inalenga kuhamasisha Washiriki na Jumuiya za Kimataifa kuhusu matumizi ya mbinu bora na teknolojia ya kisasa katika kukabiliana na kuenea kwa jangwa.

### 1.1. Kauli Mbiu ndogo

Kauli Mbiu ndogo ni kama ifuatavyo:-

1.1.1. Modern Agriculture (Kilimo cha kisasa) – Kauli Mbiu hii inalenga kuunganisha Kilimo cha kisasa na kitamaduni kwenye Mazingira ya Jangwa kwa matokeo chanya.

1.1.2. Technology and Innovation (Teknolojia na Uvumbuzi) – Kauli Mbiu hii inalenga kuwekeza kwenye teknolojia katika kilimo na kubuni njia tofauti za kilimo kwenye mazingira ya Jangwa.

1.1.3. Environment Awareness (Ufahamu wa Mazingira) – kauli Mbiu hii inalenga kukuza uelewa wa kilimo cha Mazingira ya Jangwani na uvumbuzi kwa kutoa elimu ya Mazingira hayo.

1.1.4. Sustanaibility (Uendelevu) – inalenga kuwa na mifumo ya Maisha, namna ya ufanyaji biashara na sera mbalimbali za Serikali zinazoheshimu vizazi vijavyo.

## 2.0 KAULI MBIU YA TANZANIA

Tanzania imechagua kushiriki kwenye kauli mbiu ya “Modern Agriculture” (Kilimo cha kisasa) – inayolenga kuunganisha Kilimo cha kisasa na kitamaduni kwenye Mazingira ya Jangwa ili kuleta matokeo chanya.Pia tumetengeneza kaulimbiu ndogo (Slogan) inayosema **“Teknolojia safi ya Kilimo kwa Mazingira Bora na Biashara Endelevu”** ***(“Clean Agriculture Technology for a better environment and sustainable Trade”).*** Kaulimbiu hii imeandaliwa mahsusi kwa kwa ajili ya kuifahamisha dunia namna ambavyo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilivyoamua kuipa kipaumbele sekta ya Kilimo hasa sekta ndogo ya kilimo cha matunda na mboga mboga kwa kuhamasisha matumizi ya teknolojia za kisasa na rafiki kutumia teknolojia za kisasa kwa utunzaji wa mazingira na hatimaye kuwa na biashara endelevu itakayowanufaisha watanzania.

## 3.0 AINA ZA USHIRIKI

Ushiriki wa Tanzania katika Maonesho haya umegawanyika katika maeneo makuu matatu (3) kama ifuatavyo: -

**3.1** Wizara/Taasisi za Umma;
**3.2** Taasisi za Sekta Binafsi na

**3.3** Kampuni na Wafanyabiashara

## 4.0 UTARATIBU WA USHIRIKI

### 4.1 Kushiriki katika banda la Tanzania

Washiriki kutoka Wizara/Taasisi za Umma pamoja na sekta binafsi watashiriki kwa kubadilishana (rotation) ndani ya banda la Tanzania kwa kipindi cha miezi sita (6).

| **Programu** | **Walengwa wa Programu** | Tarehe | **Tarehe ya mwisho kuwasilisha maombi** |
|---|---|---|---|
| **Matunda, Maua na Mbogamboga (Holticulture) na Mazingira** | Wawekezaji, Wabunifu, Wadau wa Teknolojia, wafanyabiashara wa matunda, maua na mbogamboga na Wizara/ Taasisi zinazosimamia sekta ya Kilimo na Mazingira | 2 Oktoba, 2023 – 28 Machi, 2024 | 30 Septemba, 2023 (Awamu ya kwanza)<br><br>30 Oktoba, 2023 (Awamu yapili)<br><br>30 Novemba, 2023 (Awamu ya Tatu) |
| **Nishati / Madini na Vito** | Wawekezaji, wafanyabiashara wa vito na madini ya viwanda, watafiti, wachimbaji, wachakataji, wachenjuaji, na Taasisi zinazosimamia madini na Nishati | 1- 30Nov, 2023 | 25 Oktoba, 2023 |
| **Utalii / Uchumi wa Buluu** | Wadau wa utalii, uwindaji, utalii wa bahari, fukwe, mambo ya kale, misitu, mazingira, Wizara/ Taasisi zinazosimamia sekta | 1 Des, 2023 – 15 Jan, 2023 | 05 Novemba, 2023 |
| **Biashara na Kilimo** | Wabunifu, Wadau wa Teknolojia, viwanda vya korosho, chai, asali, Kahawa, Katani, Viungo wadau wa kilimo, watafiti, wasafirishaji na wafanyabiashara | 15 Feb – 15 Machi, 2024 | 10 Januari, 2024 |
| **Siku ya Kitaifa** | Siku ya Kitaifa na Kongamano la Biashara | 28 - 29 Feb, 2024 | 10 Januari, 2024 |
| **Utamaduni, sanaa, usanii na ubunifu** | Wasanii, wachoraji, wachongaji, wabunifu wa mavazi, nguo, vitenge, hina, uchoraji, wanamuziki na ngoma za utamaduni na Taasisi zinazosimamia utamaduni na sanaa | 2 Oktoba, 2023 – 28 Machi, 2024 | 30 Septemba, 2023 (Awamu ya kwanza)<br><br>30 Oktoba, 2023 (Awamu yapili)<br><br>30 Novemba, 2023 (Awamu ya Tatu) |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Elimu, Ufundi na Ubunifu kwa kujifunza teknolojia** | Wanawake, Vijana na wanafunzi, wakufunzi, vyuo, mashule, Taasisi za elimu, watafiti, walemavu na wadua wa elimu | 2 Oktoba, 2023 – 28 Machi, 2024 | 30 Septemba, 2023 (Awamu ya kwanza)<br><br>30 Oktoba, 2023 (Awamu yapili)<br><br>30 Novemba, 2023 (Awamu ya Tatu) |
| **Teknolojia ya uhifadhi maji na Mazingira** | Wadau wanaosimamia utoaji wa elimu juu ya afya na matumizi bora ya maji na Mazingira Mamlaka za maji/Taasisi zinazosimamia mazingira | | |

### 4.2 Kushiriki kupitia Programu - Mikutano ya Biashara (Siku ya Tanzania)

Ushiriki wa program umegawanyika katika makundi matatu ambayo yatahusisha mikutano ya ana kwa ana baina ya Serikali kwa Serikali (G2G), Wafanyabiashara kwa Wafanyabiashara (B2B) pamoja na Serikali na Wafanyabiashara (G2B) ambapo utaratibu wa ushiriki wa mikutano ni kama ifuatavyo;-

i. Kuthibitisha ushiriki kwa kujibu barua ya Mwaliko kutoka TanTrade;
ii. Kuwasilisha majina ya maofisa/ wawakilishi pendekezwa na kuanisha mahitaji yao na kufanya Maombi ya Visa; na
iii. Mshiriki atajigharamia usafiri wa kwende na kurudi kwa njia ya ndege usafiri wa ndani, malazi, chakula pamoja na gharama nyingine.

### 4.3 Programu Binafsi

Ushiriki wa Programu Binafsi utahusisha washiriki wa Maonesho kutoka Wizara/ Taasisi za Umma, Taasisi au Jumuiya za Wafanyabiashara, Kampuni na Mtu binafsi. Washiriki hao watapaswa kuandika barua ya maombi ya kuandaliwa program katika Maonesho na kuwasilisha TanTrade kupitia barua pepe info@tantrade.go.tz program hizi zitatayarishwa kwa kushirikiana na Wadau ili kuhakikisha kuwa malengo yao yanazingatiwa.
Washiriki watakaopenda kuandaliwa program binafsi watalipa kiasi **cha Dola za Kimarekani $ 10,000** ambacho kitatumika katika uratibu wa program hiyo inayojumuisha *counterparts,* ukumbi, chakula na vinywaji. Aidha, gharama zinaweza kuongezeka kulingana na mahitaji ya mshiriki.

### 3.2.1 Matukio wakati wa Maonesho

i. Siku ya Tanzania (Tanzania National Day)
ii. Mikutano ya ana kwa ana itakayogawanyika katika makundi matatu (3) G2G, B2B, na G2B
iii. Programu za matembezi katika viwanda ili kutambua fursa za kibiashara

### 3.2.2 Ushiriki wa Maonesho

Wizara/Taasisi/Wadau wanaotaka kushiriki Maonesho ya kimataifa ya bidhaa za Kilimo Doha watafuata utaratibu ufuatao: -

i. Kupokea mwaliko na uthitisho wa ushiriki kutoka TanTrade
   a) Kuthibitisha ushiriki
   b) Kubainisha Malengo ya Ushiriki
   c) Idadi ya Washiriki
   d) Kuwasilisha taarifa (Wasifu) huduma zinazotolewa na Wizara / Taasisi/ Kampuni;

ii. Kuandaa nyaraka muhimu za safari ikiwemo Barua ya Mwaliko, Pasi ya kusafiria na viza.

iii. Kufanya utaratibu wa kuondoka kwenda Doha- Qatar.

### 3.2.3 Mambo muhimu ya kuzingatia kwa washiriki wa Program

i. Wasifu wa kampuni (company profiles) uandikwe kitaalam

ii. Kwa wenye kutafuta Wabia; Miradi iandikwe kitaalamu na kuwe na ripoti ya *feasibility study na environmental impact assessment*

iii. Wafanyabiashara wanatakiwa kuzingatia uwezo wa kuhudumia soko

iv. Kampuni iwe imesajiliwa na kupata Leseni ya Class A

v. Bidhaa ziwe na vyeti vya ubora na Cheti cha Uasili (certificate of origin)

### 3.2.4 **Sifa za Washiriki**

Mwombaji anatakiwa kuwa na sifa zifuatazo: -

i. Awe na Kampuni iliyosajiliwa kwa mujibu wa Sheria za Tanzania;

ii. Awe na Leseni hai ya kufanya biashara;

iii. Awe na vibali vinavyomruhusu kufanya biashara (madini, maliasili, afya, nishati, kilimo, utalii) kutoka kwa Mamlaka husika;

iv. Awe na uwezo wa kufanya biashara za Kimataifa;

v. Awe na Namba ya Mlipa Kodi kutoka TRA;

## 4.0 GHARAMA ZA USHIRIKI KWA KATIKA MAONESHO YA KIMATAIFA YA MAZAO YA KILIMO (HORTICULTURAL EXPO DOHA 2023)

| Na. | Tukio | Kiasi cha makadirio ya Gharama (US $) kwa mshiriki |
|---|---|---|
| 1. | **Usafiri** | |
| | Tiketi ya ndege DSM – Doha - DSM (Economy Class) | Inategemea na usafiri utakaotumia (Qatar Airways, Fly Dubai, Ethiopian Airline na Oman Air |
| | Tiketi ya ndege DSM – Doha- DSM (Business Class) | Inategemea na usafiri utakaotumia (Qatar Airways, Fly Dubai, Ethiopian Airline na Oman Air |

| | | |
|---|---|---|
| **2.** | Gharama ya Malazi | US $ 80.00 – 100 kwa siku |
| **3.** | Gharama za Usafiri Doha Qatar | US $ 3.00 kwa siku |
| **4.** | Gharama ya Visa | US $ 50 *single entry* and 100 *double entry* |

**5.0 UTARATIBU WA USAFIRISHAJI MIZIGO**

Kila mshiriki anapaswa kujaza fomu ya orodha za bidhaa (packing list) zitakazoenda katika Maonesho na kuwasilisha TanTrade kupitia barua pepe Baraka.peter@tantrade.go.tz, au baltazari.erro@tantrade.go.tz kabla ya tarehe 30 Septemba, 2023. Fomu hii inapatikana kupitia tovuti ya TanTrade www.tantrade.go.tz au kuwasiliana na namba zilizowasilishwa katika sehemu ya (8:1, 8:2)

**6.0 TARATIBU ZA VISA NA ACCREDITATION (ALO)**

Kila mshiriki anapaswa kuwasilisha nakala ya Pasi ya Kusafiria pamoja na picha (passport size) kwa ajili ya taratibu za kupata tiketi (exhibitor badge/Accreditation pass) itakayomwezesha kuingia katika eneo la Maonesho (Expo site). Taarifa hizo ziwasilishwe kwa Accreditation Liason Officer (ALO) ambaye ni Baltazari Joseph Erro kupitia barua pepe baltazari.erro@tantrade.go.tz au simu Namba +255765 823647.

**7.0 TARATIBU ZA AFYA**

Inashauriwa kila mshiriki kufanya yafuatayo kabla ya kuanza safari Qatar

- Chanjo ya Uviko 19 (Covid 19)
  *It is recommended that all visitors to Qatar are fully vaccinated against Covid 19 including all booster doses*
- Chanjo ya Mafua (Seasonal Influenza vaccination before arrival)
- Kundi la damu (Blood type)

**8.0 UTARATIBU WA KUTUMA MAOMBI YA USHIRIKI KATIKA MAONESHO YA KIMATAIFA YA MAZAO YA KILIMO (HORTICULTURAL EXPO DOHA 2023)**

Maombi yote yatumwe kwa kutumia anuani ifuatayo: -

Mkurugenzi Mkuu,
Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade),
S.L.P 5402,
**DAR ES SALAAM.**
**Barua pepe:** info@tantrade.go.tz;

8.1 **Waratibu**

Dorothy Urio +255 764 380 095, barua pepe; Dorothy.urio@tantrade.go.tz
Clara Mwamba +255 716 307590 barua pepe clara.mwamba@tantrade.go.tz,

Cecilia E. Mwandepa +255717 478806, barua pepe; cecilia.mwandepa@tantrade.go.tz

8.2 **Mratibu Dawati la Zanzibar**
Tahir Ahmed +255 7773 200 735, barua pepe; tahir.ahmed@tantrade.go.tz,

**NB:** Au fika Ofisi zetu zilizopo Uwanja wa Maonesho wa Mwl. J.K. Nyerere, Barabara ya Kilwa Dar es Salaam, Ofisi za Kurugenzi ya Biashara, Mtaa wa Malindi Zanzibar, Jengo la Kilimo V, Barabara ya VETA, Dodoma.

## 9.0 MANUFAA YA USHIRIKI

9.1 Kupata nafasi ya kuonesha bidhaa mbalimbali zinazozalishwa nchini Tanzania
9.2 Kupata fursa ya kuunganishwa na wanunuzi wa bidhaa za kilimo na mazingira
9.3 Kupata fursa ya kujifunza teknolojia mbalimbali za kilimo na mazingira
9.4 Kuwekaza katika sekta ya Kilimo na Mazingira
9.5 Kutoa fursa kwa Makampuni kujitangaza na kunadi bidhaa na huduma zinazopatikana nchini ili kupata masoko endelevu;
9.6 Kutangaza vivutio vya Kitalii vilivyopo nchini; na
9.7 Kutangaza lugha ya Kiswahili, utamaduni na desturi za Watanzania;

## 10.0 MAMBO MUHIMU YA KUJUA KUHUSU NCHI YA DOHA

| | |
|---|---|
| **Jina la Nchi:** | Qatar |
| **Mji Mkuu:** | Doha |
| **Idadi ya Watu:** | 2,717,801 |
| **Eneo:** | Al Bidda Park |
| **Lugha Kuu:** | Kiarabu na Kiingereza |
| **Pato la ndani (GDP):** | 246.79 Bilioni |
| **Dini:** | Kiislamu |
| **Sarafu:** | Qatari Riyal |

**Kiwango cha Ubadilishaji wa Fedha:**

| | | |
|---|---|---|
| 1 US $ | = | TZS. 2245 (BOT 21/07/2023) |
| 1 QR | = | TZS. 600 – 660 (BOT 21/07/2023) |
| 1 US $ | = | QAR. 3.64 |

**Hali ya Hewa:**

- Joto Kali (34.5$^0$C); Miezi ya Oktoba hadi Novemba, 2023
- Baridi (20$^0$C); Miezi ya Disemba, 2023 hadi February, 2024